

02.04.2026

TANGAZO LA ZABUNI YA UGAVI WA SHAJARA (STATIONARY) MSIMU 2025/2026

Zabuni na: KCU/G/2026/2027/06

1. KCU (1990) LTD inakaribisha maombi kutoka kwa maduka ya kuuza shajra kwa mzabuni wa kuuzia KCU vifaa hivyo kwa msimu 2026/2027.
2. Kampuni/Mtu binafsi anayeambulika anakaribishwa kuleta maombi ya zabuni hii ili kutoa huduma ya shajara kwa msimu 2026/2027.
3. Mwombaji awe na leseni ya biashara, TIN na VRN
4. Mwombaji aambatishe nakala ya wasifu wa kampuni
5. Mwombaji aambatishe nakala zinaoonesha vielelezo vya kazi alizowahi kufanya.
6. Mwombaji aambatishe nakala ya kusajiliwa na mamlaka inayotambulika.
7. Ombi la zabuni liwe na jina, anwani halisi ya mwombaji na mahali Ofisi ilipo. (Physical address)
8. Maombi yaambatane na ada ya TShs. 200,000/= ambazo hazitarejeshwa kwa mwombaji. Fedha hizo zilipwe kupitia A/C Namba **01J1055955002 General A/C**
9. Mwombaji afike Ofisi ya Manunuzi KCU (1990) LTD kupata orodha ya shajara zitakazohitajika.
10. Tathmini itafanywa kwa kuzingatia vigezo 3-8 vilivyo tajwa hapo juu.
11. Bahasha ya maombi zifungwe vizuri kwa Lakiri na kuandikwa juu yake: - **"MAOMBI YA ZABUNI YA UGAVI WA SHAJARA (STATIONARY) MSIMU 2026/2027"** kwa anwani tajwa hapa chini,

MENEJA MKUU,
KCU (1990) LTD,
P.O BOX 5,
BUKOKA.

12. Bahasha hiyo iletwe kwa mkono katika Ofisi ya Manunuzi KCU kabla au mnamo tarehe 20.04.2026 saa 4.00 asubuhi siku ya Jumatatu na ufunguzi wa maombi yote utafanyika muda huo, waombaji au wawakilishi wa waombaji wanaalikwa katika sherehe ya ufunguzi mara tu baada ya saa ya mwisho yakupokea zabuni.
13. Maombi yatakayochelewa, maombi yasiyokamilika, maombi yaliyowasilishwa kwa njia ya kieletroniki na maombi yasiyokuwepo siku ya ufunguzi hayatahusishwa na uchambuzi wa kumpata mzabuni.

Imetolewa na;

